Sisi ni nani?

Concertation-Femme ni shirika bila faida inasaidia wanawake wa Bordeaux-Cartierville na wa jirani. Ni fasi ine wa karibisha, ni fasi inasikiliza lazima ya wanawake, na ni fasi pale wanawake wote wanaweza kukutana, kuongea na kujenga jamaa ya kusaidiana. Kuna fasi ya bure ya kulinda watoto kiloko kwa wanawake wana simamia ma shuguli zetu.

Ujumbe yetu

Kazi ya shirika yetu ni ya ku fanya ya kama maisha ya wanawake igeuke vizuri mu kuondosha maisha ya upweke na kuwasaidia wapate uhuru mu fedha, mu kipendo na mu jamaa.

Ustawi yenu ni sababu zetu ya kwishi…

Huduma na kile tunachofanya

- Masomo ya kifaransa
- Huduma ya kukaribisha na kusaidia
- Huduma ya halte-garderie
- Darasa ya maendelezo binafsi
- Darasa ya ba mama
- Darasa juu ya afya ya wanawake
- Darasa ya kazi ya mkono
- Maelezo ya kisheriwa

Kutufikia

1405, boul. Henri-Bourassa O, ofisi 012
Montreal (Québec) H3M 3B2
Simu : 514 336-3733
info@concertationfemme.ca
www.concertationfemme.ca
Tufuate pa

CONCERTATION FEMME

Ma namna ya kulinda watoto hapa Quebec

Habari kwa wazazi wa nafika sasa inchi hii

(Swahili)

Montreal, 2019

Huduma ya kulinda watoto ya ubora

Hati hii ni ya nani?

Hati hii inaangalia wazazi na wale wanafika sasa nchii hii na ina kazi yaku wasaidia ku chagua ma fasi ya kulinda watoto wao kufatilia imani na lazima yao.

Kwa nini ni lazima kuchagua fasi ya kulinda watoto ya ubora?

Miaka ya kwanza ya maisha ya mtoto ni muhimu kwa maendelezo wake binafsi.

Hivyo, inahitaji msisitizo ili kukuza maendeleo yake katika vipimo vitano (ufahamu, kutembea, lugha, na ujamii na kipendo).

Hivyo, mtoto ambaye anaenda kwenye fasi ya kumulinda ya ubora atakuwa tayari tayari kwenda shule.

Kujua kwamba huduma ni ya ubora

Wazazi hawapaswi kusita kutembelea ile mafasi na kuuliza maswali kuhusu programu ya elimu na mafunzo ya wafanyakazi kabla ya kukamata uamuzi. Kufatilia mambo yaliyo chini :

- Namba wafanyakazi/watoto :
  - ❖ Wafanyakazi moja kwa watoto 5 ao chini, chini ya miezi 18; Wafanyakazi 1 wa watoto 8 au chini, miezi 18 mpaka chini ya miaka 4; Wafanyakazi 1 kwa watoto 10 au chini, wenye umri wa miaka 4 mpaka chini ya miaka 5 mnamo Septemba 30;
  - ❖ Wale wanalinda watoto mu ma nyumba zao, sheria inaomba kwa mufanyakazi moja inapasua watoto 6 (watoto mchanga 2) ao kwa wafanyakazi wawili inapasua watoto 9 (watoto mchanga 4);
- Wafanyakazi walisoma namna ya kulinda Watoto;
- Chumba na hawa, safi, ndani pale jua ina ingia;
- Chakula mzuri kwa mwili hasa matunda na mboka za majani;
- Shughuli na maingilio kwa watoto ina heshimia kanuni za mpango wa Elimu ya Familia.

Kazi ya huduma ya ubora juu ya maendeleo ya watoto

Majifundjo ya ningi inaonesha faida ya huduma ya kulinda watoto juu ya maendeleo ya watoto kwenye watoto wana toka fasi bila feza mingi na juu ya watoto wanakuwa na hali nguvu. Hata hivyo, huduma inapaswa kuya ya ubora.

Huduma ya ubora inasaidia mtoto kuwa na wa rafiki**,** kuendeleza ujuzi yake**,** kupanua lugha yake na hamu yake ya kujifunza, kuhakikisha usalama na ustawi yake, kutambua na kujibu mahitaji ya watoto.

Programu ya elimu

Programu ya elimu ina lengo :

- Kupa watoto huduma ya ubora;
- kutumikia kama chombo cha kumbukumbu kwa mtu yeyote anayefanya kazi katika sekta ya huduma ya watoto;
- kuchunga umoja katika ma huduma ya watoto wengi.

Kanuni za msingi za programu ya elimu:

- **Kila mtoto eko pekee katika aina yake**, na programu ya elimu ina lazima kuheshimu kasi lake ya maendeleo, lazima yake na shamba la masilahi;
- **Mtoto ni ajanti ya kwanza ya maendeleo yake,** ni kusema ya kwamba maendeleo inatoka na mwelekeo iko ndani ya watoto. Wafanya kazi wanasaidia tu watoto kuwapeleka mpaka uhuru.
- **Maendeleo ya watoto ni ikubwa** na vipimo nyingi : mu kipendo, mu mwili na kutembea, mu ujamii na mu adili, mu ufahamu na luga.
- **Mtoto anajifunza kwa mchezo**, ni shughuli kuu ya huduma ya watoto.
- **Ushirikiano kati ya walimu** au wale wana kuwa na huduma za watoto nyumbani na **wazazi** ni muhimu kwa maendeleo ya usawa ya mtoto**.**

Shauri ya chakula ya Kanada

Shauri ya chakula ya Kanada ni chombo ilioletwa na Afya ya Kanada.

Kwa maelezo zaidi, tembelea tovuti: **https://guide-alimentaire.canada.ca/fr/**

Maneja ya huduma ya watoto nyumbani ya ruzuku anaweza kuandika yeye peke mapatano ya huduma ao kutumia mfano ya wizara.

Maneja ya huduma ya watoto ya ruzuku anaweza ku ghairi mapatano kwa mujibu wa masharti yaliyowekwa katika ile mapatano.

Ule maneja ya huduma isiyofadhiliwa ao maneja ya huduma ya watoto nyumbani isiyofadhiliwa , anaweza ku ghairi mapatano wakati wazazi wakati wazazi hawatimiza majukumu yao, kwa mfano, si kulipa fedha imeombwa

Chakula

CPE, huduma ya ruzuka na huduma isiyofadhiliwa na huduma ya watoto nyumbani ya ruzuku inapaswa kuwapa watoto ma chakula mbili kidogo na chakula moja kubwa.

Ni lazima ba :

- hakikishe kwamba ile machakula inafuata **shauri ya chakula ya Kanada**;
- fuate ma shauri ya wazazi juu ya machakula ya watoto, kama ameagizwa chakula maalum kilichowekwa na mganga, wanachama wa Chuo cha Quebec;
- kuchunga na kutumikia chakula chini ya hali ya usafi na kwa joto linalofaa;
- kuonyesha menyu ya kila wiki kwa kushauriana na wafanyakazi na wazazi. Kumbuka kwamba maneja ya huduma ya watoto wa nyumbani si lazima kuonyesha menyu, lakini lazima akujulishe yaliyomo ya chakula na vitafunio
- Mtoa huduma ya watoto, pamoja na kuunda menyu na afya, anaendeleza tabia za kula ya safi na kuzingatia mizigo na kutovumilia chakula.

Utaratibu ya lawama

Wazazi wanaweza kulalamika ikiwa hawana furaha na huduma ya watoto; juu ya :

- Masaa ya kufunguliwa;
- Usafi ya chumba ;
- Uhusiano wa mzazi na huduma ya watoto;
- Afya na usalama wa watoto katika huduma;
- Sio kufuata namba uliowekwa na wizara, na vingine.

Wazazi wanaweza kufanya lawama

Kwa simu :
mufikie mstari wa habari usio na malipo katika 1-855-336-8568

Kwa barua :
kutuma lawama ku :
Bureau des plaintes et de l'amélioration de la qualité
Ministère de la Famille
600, rue Fullum, Sakafu ya 5
Montreal (Québec) H2K 4S7

Gharama na mambo mengine

Mapato ya familia ni nini?

Mapato ya familia ni mapato halisi ya mwaka uliopita.

ukiwa una mke, mapato yako ya familia ni mapato halisi yako pamoja na yale ya mwenzi wako.

Kwa habari juu ya suala hili, wasiliana wizara ya familia : **www.mfa.gouv.qc.ca/fr/Pages/index.aspx**

Usisahau ….

Wazazi wanaweza kughairi mapatano ya huduma wakati wowote na kwa hiari yao. Wanaweza kutuma taarifa iliyoandikwa au fomu ile inapatwa mu « Loi sur la protection du consommateur »

Programu ya mafasi ya kulipa fedha kidogo

Hii programu inasaidia wa zazi kulipa fedha yenye kupunguzwa juu ya watoto mu huduma ya watoto. Hii mafasi iko mu ma CPE, mu Huduma ya ruzuku na mu huduma ya watoto nyumbani ya ruzuku. Kama mfano, hapa ni kiasi cha mwaka 2019.

Wazazi walipashwa kulipa dola 8,25 ku siku kwa mtoto mu huduma ya fedha yenye kupunguzwa. Kama mapato ya familila ilipita dola 52 220, wazazi walipashwa kulipa malipo ya ziada.

Malipo wa ziada unabadilika kufuatana na mapato halisi ya familia kama ifuatavyo:

Mapato halisi ya familia kwa mwaka uliopita	Malipo wa ziada kwa siku kwa mutoto wa kwanza	Malipo ya kila siku
Dola 52 220 ao chini	Hakuna	Dola 8,25
Kutoka dola 52,220 hadi 78,320	Dola 0,70	Dola 8,95
Kutoka dola 78 320 hadi dola 166 320	Kati ya dola 0.70 na dola 13.90	Kati ya dola 8,95 na dola 22,15
Dola 165 006 $ ao juu	Dola 13,90	Dola 22,15

Mtoto wapili : malipo wa ziada imepunguzwa kwa 50%

Mtoto wa tatu na wengine : hakuna malipo wa ziada

Malipo ya kila siku ya dola 8,25 kwa mtoto inacholipwa kwa huduma ya ruzuku

Malipo wa ziada yote uliohesabiwa nyuma ya mapato ya familia italipwa kwa Revenu Québec, wakati yakutangaza kodi mu « relevé 30 », ambayo lazima inapaswa kutolewa siku ya mwisho ya Februari.

Wazazi wanaopata msaada wa usaidizi wa kifedha kwa Kazi, Ajira na Ushirikiano wa Jamii hawalipe fedha chochote. Na vile wale wazazi wanaopata usaidizi ya « Programme objectif emploi et du Programme de sécurité du revenu des chasseurs et piégeurs cris », hawalipe chochote. Na wale wanaopata usaidizi ya « Programme d'aide sociale, du Programme de solidarité sociale et du Programme alternative jeunesse » hawalipe nawo pia.

Mapatano kati ya wazazi na huduma ya kulinda watoto.

Mapatano inapashwa kuwa kati hata moja wa wazazi na maneja wa huduma.
Kuna aina 2 za mapatan:

1. « Mapatano ya huduma ya watoto ya ruzuku juu ya mtoto chini ya umri wa miaka 5 hadi Septemba 30». Hii mapatano ni ya huduma ya watoto na iko lazima juu ya kituo cha utoto ya rukuzu na huduma ya rukuzu. Mapatano lazima kuheshimia mahitaji ya wazazi.
2. Mapatano juu ya huduma isiyofadhiliwa iko juu ya huduma ya watoto nyumbani ingekuwa na ruzuku ao hapana.

Maneja ya huduma ya watoto nyumbani ao hapana, ya ruzuku ao hapana, lazima awe na mapatano na wazazi, mapatano imeitwa « de contrat de service à exécution successive (Mapatano unaoelezea ya kwamba huduma itafanywa kwa muda mrefu au mfupi).

Aina ya mafasi ya kulinda watoto

Ni vizuri kujua …

Meneja wa huduma ya watoto lazima ape huduma za elimu na ubora wa watoto.

Anahitaji kuunda kamati ya wazazi ambayo inatoa ushauri juu ya mashida ya huduma ya watoto..

Kujua yakama…..

Huduma zote inapaswa kuwapa wazazi risiti kwa fedha zote zinazolipwa kama gharama za huduma za watoto

1. Kituo cha utoto ya ruzuku (CPE)

Ni nini?	Ni shirika bila faida ambayo yana kibali cha Wizara.
Gharama za huduma	Kuna mafasi ya bei kidogo. Malipo ya ziada zinazokubaliwa kwa wizara yanaweza kuongezwa.
Kazi ya wazazi	inaendeshwa na bao ambayo kuna angalau wanachama 7, angalau 2/3 kati yao ni wazazi ambao ni watumiaji au watumiaji wa baadaye wa CPE. Wanaweza kushiriki: – kuhakikisha usimamizi mzuri wa huduma, programu na rasilimali; – kufafanua sharti na kuweka malengo – kupitisha mpango wa elimu, na vingine.
Chakula	Vitafunyo mbili na chakula moja kubwa ku fuata shauri ya chakula ya Kanada.
Masaa ya kufunguliwa	Masaa ya ufunguzi ya hudumu ya kulinda watoto : kipindi kya kuendelea ya saa 10 kwa siku.
Mafunzo ya wafanyakazi	Wengi wanakuwa na digrii (Wafanyakazi 2 kati ya 3) : Diploma ya Chuo cha Mafunzo katika Elimu ya Watoto Mapema au uwiano mwingine wowote kutambuliwa.

2. Huduma ya ruzuku

Ni nini?	Shirika lwa faida (wengi) au shirika bila faida ambayo yana kibali cha Wizara.
Gharama za huduma	Kuna mafasi ya bei kidogo. Malipo ya ziada zinazokubaliwa kwa wizara yanaweza kuongezwa.
Kazi ya wazazi	Kamitii ya mashauri ya wazazi ina jengwa na inaweza kuleta shauri yake, hasa juu: - matumizi ya programu ya elimu; - kununua na kutumia vifaa vya elimu na vifaa vyovyote; - mpangilio na kununua fanicha; - huduma zinazotolewa - Kutazama lawama.
Chakula	Vitafunyo mbili na chakula moja kubwa ku fuata shauri ya chakula ya Kanada.
Masaa ya kufunguliwa	Masaa ya ufunguzi ya hudumu ya kulinda watoto : kipindi kya kuendelea ya saa 10 kwa siku.
Mafunzo ya wafanyakazi	Wengi wanakuwa na digrii (Wafanyakazi 2 kati ya 3) : Diploma ya Chuo cha Mafunzo katika Elimu ya Watoto Mapema au uwiano mwingine wowote kutambuliwa.

Jinsi gani kuomba mikopo ya kodi ya gharama ya kulinda watoto?

Mzazi anayeweza kulomba anaweza kuomba mikopo ya kodi ya kulinda watoto:

- wakati wa kutaganza kodi zake;

- wakati wowote wa mwaka, ikiwa anataka kuipata kabla..

Kwa habari juu ya suala hili, wasiliana na **Revenu Québec.**

3. Huduma isiyofadhiliwa

Ni nini?	Shirika lwa faida (wengi) au shirika bila faida ambayo yana kibali cha Wizara.
Gharama za huduma	Hakuna mafasi ya bei iliyopunguzwa. Ana bei yake yepeke. Mzazi anapewa taarifa ya kodi juu ya wakati yakutangaza kodi.
Kazi ya wazazi	Kamitii ya mashauri ya wazazi ina jengwa na inaweza kuleta shauri yake, hasa juu: - matumizi ya programu ya elimu; - kununua na kutumia vifaa vya elimu na vifaa vyovyote; - mpangilio na kununua fanicha; - huduma zinazotolewa - Kutazama lawama.
Chakula	Vitafunyo mbili na chakula moja kubwa ku fuata shauri ya chakula ya Kanada.
Masaa ya kufunguliwa	Kwa busara ya huduma ya watoto
Mafunzo ya wafanyakazi	Wengi wanakuwa na digrii (Wafanyakazi 2 kati ya 3) : Diploma ya Chuo cha Mafunzo katika Elimu ya Watoto Mapema au uwiano mwingine wowote kutambuliwa.

4. Huduma ya watoto nyumbani ya ruzuku

Ni nini?	Huduma ya watoto nyumbani inakuwa ndani ya nyumba ya mtu moja na ni lazima awe kutambuliwa na mamlaka ya huduma ya watoto. Mtu anayejulikana akifanya peke yake, anaweza kutoa huduma ya watoto kwa watoto hadi sita, ambao wawili wanaweza kuwa na umri wa chini ya miezi 18. Ikiwa amesaidiwa na mtu mwingine mzima, anaweza kupokea watoto saba hadi tisa, lakini si zaidi ya watoto wanne chini ya miezi 18 ya umri.
Gharama za huduma	Kuna mafasi ya bei kidogo
Kazi ya wazazi	Hakuna
Chakula	Vitafunyo mbili na chakula moja kubwa ku fuata shauri ya chakula ya Kanada
Masaa ya kufunguliwa	Masaa ya ufunguzi ya hudumu ya kulinda watoto : kipindi kya kuendelea ya saa 10 kwa siku.
Mafunzo ya wafanyakazi	Saa 45 ya kujifunza na saa 6 ya kuboresha kila mwaka

5. Huduma inaitwa « Halte-garderie » ya jamii

Ni nini?	« Halte-garderie » ya jamii ni huduma inayotolewa na shirika la jamii linalotumikia wa familia zinazo watoto wadogo. Ni huduma ya wakati mfupi ao ya kusaidia. Wengi wa « Halte-garderie »wanakua na programu ya elimu yabo peke.
Gharama za huduma	Huduma ya bure ao kila « halte-garderie » ina malipo kwa saa.
Kazi ya wazazi	Hakuna
Chakula	Kila « halte-garderie » inachagua chakula yake.
Masaa ya kufunguliwa	Kila « halte-garderie » inachagua masaa yake.
Mafunzo ya wafanyakazi	Kila « halte-garderie » inachagua elimu yake.

6. Huduma ya watoto nyumbani inayotolewa na mtu asiyejulikana

Ni nini?	Mtu anaweza kutoa huduma ndani ya nyumba yake kwa watoto hadi sita (6), ambao si zaidi mbili wana kuwa chini ya miezi kumi na nane (18), ikiwa ni pamoja na watoto chini ya umri wa miaka tisa ambao wana ishi pamoja naye na ambao wanapo wakati wa utoaji huduma. Hii huduma haijatambuliwa na mamlaka ya huduma ya watoto.
Gharama za huduma	Hakuna mafasi ya bei iliyopunguzwa. Ana bei yake yepeke. Mzazi anapewa taarifa ya kodi juu ya wakati yakutangaza kodi.
Kazi ya wazazi	Hakuna
Chakula	Kwa busara ya huduma ya watoto
Masaa ya kufunguliwa	Kwa busara ya huduma ya watoto
Mafunzo ya wafanyakazi	Inategemea

Ufikiaji moja kwa huduma za huduma za watoto

Tembelea,: www.laplace0-5.com, ao ita
514 270-5055,
1 844 270-5055

Wazazi wanapata je huduma ya watoto

Idara ya Familia imeunda fasi moja juu ya wazazi waandikishe watoto ku huduma ya watoto, iitwayo **La Place 0-5**. **La Place 0-5** inaruhusu wazazi kuandikisha mtoto wao mu huduma vyote, huduma ya ruzuku, huduma isiyofadhiliwa na huduma nyumbani yenye kutambuliwa. Wazazi wanaweza kujiandikisha mtoto wao katika La Place 0-5 hata kabla ya kuzaliwa.

Tangu 18 Juni, 2018, wazazi wanaweza kuona kwenye ramani, ma CPE, huduma ya watoto yote ambazo zinatambuliwa huko Quebec.

Tangu Septemba 1, 2018, CPE zote, Huduma ya watoto zote wamejiunga na La Place 0-5 na wanatumia usajili wa wazazi juu ya kuongeza watoto ndani ya shirika yao.